JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
(TAMISEMI)
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA
SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI MUSOMA.
S.L.P 54 Musoma.
Simu:0787 985030, 0752 985030.
E-mail:musomatechsecondaryschool@gmail.com
Web site: www.musomatech.sc.tz

YAH: MWANAO KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI MUSOMA MWAKA 2022.

Ninayo furaha kukujulisha kuwa mwanao …… amechaguliwa kujiunga na Kidato cha **V** mwaka **2022** katika shule hii ambapo atapata Elimu na hatimaye kujitegemea na kulitumikia Taifa. Kama Mzazi/Mlezi unapaswa kumuasa mwanao azingatie masomo pamoja na taratibu zote za shule na kumpa mahitaji yote ya shule ili aweze kufanikisha azma hii.

Shule ya Musoma Sekondari ya Ufundi iko katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma Mkoani Mara, umbali wa Kilomita 4 kutoka Makao Makuu ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma. Kutokea Stendi kuu ya Mabasi ya Bweri, barabara iendayo Musoma Mjini, kuna kibao kinachoitambulisha shule upande wa kushoto.

Shule itafunguliwa Muhula wa kwanza tarehe **……..** Muda wa kuripoti ni kuanzia **saa 02:00 Asubuhi** hadi **saa 12:30 jioni.** Mwanafunzi anatakiwa kuwa ameripoti shuleni kuanzia tarehe ya kufungua na mwisho wa **kuripoti itakuwa wiki mbili tokea tarehe ya kuripoti**. Mara mwanafunzi afikapo shuleni **aripoti Ofisini kwa Makamu Mkuu wa Shule kwa mapokezi na usajili.** Makamu Mkuu wa shule atahakikisha kwamba mwanafunzi amekuja na "Pay in Slip" tatu zilizolipiwa kwenye **Akaunti za Shule zilizoko katika Benki ya NMB kama ifuatavyo; Ada ya Shule ilipwe kwenye Akaunti Namba 30301100105 yenye jina MUSOMA TECHNICAL SECONDARY SCHOOL (RECURRENT ACCOUNT),** fedha za michango mingine ya shule zilipwe kwenye **Akaunti Namba 30301100043 yenye jina MUSOMA TECHNICAL SECONDARY SCHOOL na fedha kwa ajili ya Ukarabati wa Miundo mbinu na Samani zilipwe kwenye Akaunti Namba 30301200414 yenye jina MUSOMA TECHNICAL SECONDARY SCHOOL (DEVELOPMENT ACCOUNT).** Fedha za matumizi binafsi ya mwanafunzi zisiwekwe kwenye Akaunti za Shule bali aje nazo mkononi.

Pia mwanafunzi ajapo shuleni ni muhimu aje na vitu vifuatavyo;

i.Kivuli cha Cheti cha Kuzaliwa kinachotolewa na Serikali (copy of Birth Certificate).
ii. Fomu iliyojazwa na Daktari kuhusu Afya ya Mwanafunzi (Medical Examination Form).
iii. Fomu iliyojazwa ya maelezo binafsi ya mwanafunzi (Personal Particularas Form).
iv. Fomu ya kukubali masharti ya shule. Wewe na mwanao muisome kwa kina pamoja na sheria za shule mkizikubali, msaini fomu hizo na ziwasilishwe shuleni hapa wakati wa kuripoti.
v. Kivuli cha Cheti cha kumaliza Kidato cha Nne (Leaving Certificate).
vi. Kivuli cha matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Nne (Result Slip) .
vii. **Picha nne (04) "Passport Size" za Mwanafunzi na Picha moja moja "Passport Size" za Wazazi na ndugu wa karibu wa Mwanafunzi wanaoweza kumtembelea Mwanafunzi au kuitwa wakati wa Matatizo mbalimbali pamoja na namba zao za Simu.**

Ndugu Mzazi/Mlezi, Shule hii haina utaratibu wa chakula maalum (Special diet) kwa mwanafunzi mmoja mmoja tofauti na kile kinachoandaliwa kwa ajili ya wanafunzi wote. Vile vile shule ina mihula miwili (02) ya masomo na kila muhula unapokwisha shule huwa inafungwa. Hivyo mzazi unatakiwa kumtumia mwanao nauli ya kurudi nyumbani kwa ajili ya mapumziko. Shule hairuhusu mwanafunzi kubaki shuleni wakati wa likizo. Pamoja na barua hii naambatanisha orodha kamili ya vifaa vya lazima mwanafunzi anavyopaswa kuja navyo na fomu mbili anazotakiwa kujaza na kuja nazo wakati wa kuripoti shuleni.

..
MKUU WA SHULE
Mawasiliano - 0787 985030 (Mkuu wa Shule) na 0621 351543 (M/Mkuu wa Shule).
0755 671818 (Mwandamizi Taaluma)

i. Karo ya Shule Tsh. **70,000/=** kwa mwaka au TSh. **35,000/=** kwa muhula – Ziwekwe **Akaunti Namba. 30301100105 NMB.**

ii. Taaluma Tsh. 30,000/= kwa kila mwaka. **-Akaunti Namba. 30301100043 - NMB**

iii. Matibabu Tsh. 15,000/= kwa kila mwaka. - **Akaunti Namba. 30301100043 - NMB**

iv. Ulinzi,Wapishi na vibarua wengine Tsh. 30,000/= kwa kila mwaka- **Akaunti Namba. 30301100043 - NMB**

v. Fedha ya Tahadhari Tsh. 5,000 (Hairudishwi) - Akaunti Namba. 30301100043 – NMB

vi. Mitihani endelezi Tsh.15,000/= Akaunti Namba. 30301100043 - NMB

vii. Fedha za **Kitambulisho na Picha Tsh. 6000/= -Aje nayo taslim**

viii. Tsh. 2,000/= kwa ajili ya **Nembo ya Shule** . **- Aje nayo taslim**

xi. Ukarabati wa Miundo mbinu na Samani Tsh. 15,000/= ziwekwe Akaunti Namba 30301200414 - NMB

JUMLA - TSH.188,000/=

SARE YA SHULE. Sare ya shule hii ni;

- Mashati mawili meupe yenye **mikono Mirefu**.
- Suruali mbili nyeusi zenye mifuko miwili ya pembeni na mmoja nyuma kulia zisizobana na zisiwe **"Jeans"** wala **"Modo"** Upana wa chini usipungue **inchi "15" ukipungua hiyo suruali itachanwa.**

Tshirt mbili (2) za kushindia baada ya masomo rangi ya blue zenye kola nyeusi na vishikizo vitatu visivyo na maandishi.

MUHIMU: Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kuwa na nguo za nyumbani shuleni.

- Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba jozi 2 visiwe na kisigino kirefu wala shingo ndefu.
- Soksi jozi 2 rangi nyeusi.
- Sweta ya rangi ya kijani kibichi (Rangi ya mimea) yenye alama ya "V" shingoni.
- Suruali ya rangi ya damu ya Mzee– huvaliwa baada ya saa za masomo.
- Aje na viatu na nguo za michezo. Bukta na Tshirt ya rangi ya Blue kwa Kidato cha Tano, traki suti ya bluu bahari.
- Mkanda wa ngozi rangi nyeusi au ugolo wa ukubwa wa kati usio na "bicross" kubwa.
- Tai mbili nyeusi **(Zinapatikana maeneo ya shule.)**

NB. Mwanafunzi wa shule hii hapaswi kuja na nguo nyingine yoyote tofauti na hizo hapo juu. Nguo za nyumbani hazitakiwi kabisa shuleni hapa.

VIFAA VYAKE BINAFSI VYA KUTUMIA BWENINI

1. **Godoro** la **"Sponge" la 2.5ft x6"x6" (**Zinapatikana maeneo ya shule endapo utashindwa kupata huko uliko**).**
2. Shuka mbili mpya rangi moja ya bluu bahari (Light blue).
3. Mto na foronya ya rangi ya blue bahari.
4. Chandarua (Vitanda vyetu ni Futi 2.5)
5. Ndala/Kandambili
6. Taulo
7. Sanduku la bati kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake ni (lazima)
8. Ndoo moja ya kuchotea maji na dumu la lita 5 kwa ajili ya kutunzia maji yake ya kunywa (Lazima).
9. Mwanafunzi aje na Toilet paper walau 10 kwa matumizi yake.
10. Sahani, bakuli, Kijiko na Kikombe cha nusu lita .
11. Fedha za matumizi yake muhimu ya kila siku na nauli ya kurudi nyumbani wakati wa likizo au dharura.

VIFAA VYA KUTUMIA DARASANI NA WAKATI WA MITIHANI

1. Ream ya Karatasi A4 mbili(**AINA YA DOUBLE "A" (Ni lazima kila mwaka).**

2. Mathematical set

3.Kamusi (English Dictionary)

4. Madaftari makubwa (Counter Books) yasiyopungua 10.

5. Scientific calculator ya " function kuanzia fx – 82MS to fx – 991MS (Kwa Kidato cha Tano michepuo ya **PCM, PGM, EGM,CBG,PCB na HGE). (Zinapatikana maeneo ya shule endapo utashindwa kupata huko uliko).**

6. Dissecting Kit" (Kwa wanafunzi wa Kidato cha Tano – Mchepuo wa **CBG na PCB (Zinapatikana maeneo ya shule endapo utashindwa kupata huko uliko).**

SHERIA ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.

A. KILA MWANAFUNZI WA SHULE HII NI LAZIMA AZINGATIE MAMBO YAFUATAYO;

a) Heshima kwa viongozi wazazi wafanyakazi wote na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Kuhudhuria katika kila shughuli ndani na nje ya shule pale unapohitajika.
c) Kuhudhuria bila kukosa kwenye maandalio ya usiku (Night Preparation & Morning preparation).
d) Kufahamu mipaka ya shule na kuepuka kuwa nje ya mipaka ya shule bila ruhusa.
e) Kutunza usafi na mazigira ya shule wakati wote.
f) Kuvaa sare ya shule wakati wote mwanafunzi anapokuwa nje ya shule na nje ya shule.
g) Kufuata ratiba ya shule wakati wote.

B. MAMBO AMBAYO MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUFANYA

a) Kuvuta sigara.
b) Kufuga kucha ndefu, nywele ndefu na ndevu.
c) Kuvaa mavazi yasiyo sare rasmi ya shule ndani ya eneo la shule na nje ya shule.
d) Kupigana/ kuchochea ugomvi au kumpiga mtu yeyote.
e) Kuiga mitindo ya kihuni isiyofaa katika jamii.
f) Kwenda nje ya shule bila ruhusa kutoka kwa mwalimu.
g) Kumiliki simu shuleni.
h) Kula chakula nje ya Bwalo la chakula bila ruhusa.
i) Kupeleka mgeni Bwenini ama sehemu nyingine isiyohusika tofauti na maeneo yaliyoelekezwa.
j) Kwenda kwenye yumba za walimu ama watumishi wasio walimu bila ruhusa au sababu ya muhimu.
k) Kuingia au kutembelea maeneo ya kuuzia vileo na majumba ya starehe.

C. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA NI:

1. Wizi
2. **Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/Utoro.**
3. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
4. Kutoa lugha chafu kwa Wanafunzi wenzake, Walimu/Walezi na Jamii kwa ujumla.
5. Kupigana Mwanafunzi kwa Mwanafunzi,kumpiga Mwalimu au mtu yeyote Yule.
6. Kusuka/Kunyoa nywele kwa mtindo usiokubalika.Wanafunzi wakati wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo Shuleni.
7. Kufuga ndevu.
8. Ulevi au unywaji wa Pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
9. Uvutaji wa Sigara.
10. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.
11. Kushiriki matendo ya uhalifu, Siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
12. Kusababisha Mimba au kumpa mimba msichana.
13. Kudharau bendera ya Taifa.
14. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
15. Uharibifu wa Mali ya Umma kwa makusudi.
16. **Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi; kukutwa na "line" ya simu, "charger" au betri ya simu katika mazingira ya Shule.**

ZINGATIA: MWANAFUNZI ATAKAYEPATIKANA NA SIMU SHULENI ATAFUKUZWA SHULE MARA MOJA NA KULIPA FAINI YA TSH.200,000/=.

PIA SHULE YETU KWA SASA IMEFANYIWA UKARABATI MKUBWA NA SERIKALI.HIVYO MWANAFUNZI AKIJIHUSISHA NA UHARIBIFU WA MALI YA UMMA IKIWEMO KUCHAFUA KUTA KWA MAANDISHI,KUVUNJA TAA,VIOO,MILANGO N.K ATALAZIMIKA KUFIDIA GHARAMA ZA UHARIBIFU HUO.



MKUU WA SHULE

OFISI YA RAISI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA
SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI MUSOMA

FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI PAMOJA NA AHADI YA UTII WA SHERIA ZA SHULE

1. Jina kamili (Kama ilivyo kwenye TSM 9) …….
2. Anwani ya nyumbani ……..
3. Tarehe ya kuzaliwa …….
4. Mahali ulipozaliwa, Kijiji/Mtaa…… Kata……Tarafa……
   Wilaya…….. Mkoa…….
5. Mahali unapoishi kwa sasa Kijiji/Mtaa……..…….. Kata…….Tarafa……
   Wilaya…….. Mkoa…….
6. Shule ya Sekondari ulikotoka…….
   Anwani……
7. Dini/Dhehebu……..
8. Kabila…….
9. Taifa (Mtanzania/Si Mtanzania……..

10. JAMAA KATIKA FAMILIA AMBAO WANAWEZA KUPELEKEWA TAARIFA ZAKO MUHIMU KWA MASUALA YAHUSUYO SHULE:

(JAZA SEHEMU ZOTE NNE, PAMOJA NA PASSPORT SIZE ZA KILA MZAZI/MLEZI)

i) **Jina la Baba**…… Namba ya Simu ……
Anaishi/ Haishi…….
Kazi yake……..……
Anwani……
PICHA

ii**) Jina la Mama**…… Namba ya Simu ……
Anaishi/ Haishi…….
Kazi yake……..……
Anwani……
PICHA

iii) **Jina la Mlezi (1)**……Uhusiano……Namba ya Simu ……
Kazi yake……
Anwani……
PICHA

iv) **Jina la Mlezi (2)**…… Uhusiano……Namba ya Simu ……
Kazi yake ……
Anwani……..……...
PICHA

Mimi (Mwanafunzi)…….. nathibitisha kuwa taarifa nilizozijaza hapo juu ni za kweli. Ahadi yangu, Nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga na shule hii na ninahaidi kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyotolewa na zitakavyotolewa na uongozi wa shule.

…… ……..
Sahihi ya Mwanafunzi Tarehe

Mimi (Jina la Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi)…….. ambaye ni Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi …… nimeyasoma masharti na sheria za shule ya Sekondari Musoma ambako kijana wangu amechaguliwa kujiunga. Nahaidi kwamba nitamuhimiza mwanagu kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyoelezwa. Aidha nahaidi kushirikiana na uongozi katika malezi bora ya mwanagu ili baadae awe raia bora na mwema wa Taifa letu.

……

…….
Sahihi ya Mzazi/Mlezi Tarehe

MUSOMA TECHNICAL SECONDARY SCHOOL
MEDICAL EXAMINATION FORM
MUSOMA TECHNICAL SECONDARY SCHOOL, P.O BOX 54, MUSOMA. Date……

To Medical Officer, …… …… ……
Ref…….. (NAME OF STUDENT)

Please examine the named Student as per Medical examination form below,



MOHAMED B. KAJERI
HEADMASTER

MEDICAL EXAMINATION FORM

(To be completed by Government Medical Officer) Full Name……..
Age…….Height……(cm)Weight……..(Kg)

1. Blood count (Red and White)……

2. Stool Examination……..

3. Urinary analysis……

4. STDs and other V.D.....

5. T.B and Leprosy test……...

6. Eye test……

7. Ear test……

8. Chest …….

9. Abdominal test…….

10. Blood Group **(Very Crucial)**……

11. Spleen…….

Any additional defects or impairments, infections, chronic or family diseases (e.g Sickle cell),
……..……...……
……
……
……. I have examined the above named student and I certify that he/she is FIT/NOT FIT to pursue Secondary Education.
Signature…….Date…….
Station……
Designation and Official Stamp…….

THANK YOU

VIFAA VYA USAFI ANAVYOPASWA KUNUNUA MWANAFUNZI KULINGANA NA TAHASUSI ALIYOCHAGULIWA.

Na.	TAHASUSI	JINA LA KIFAA.	IDADI
1	PCM	JEMBE LENYE MPINI	01
		SLESHA	01
		SOFT BROOM	01
2	PGM	Shear (GRASS CUTTER)	01
			01
			01
3	CBG	JEMBE LENYE MPINI	01
		SLESHA	01
		SOFT BROOM	01
4	EGM	JEMBE LENYE MPINI	01
		REKI	01
			01
5	HGE	SOFT BLOOM	
		SHEAR(GRASS CUTTER)	01
			01
6	HGK	SOFT BROOM	01
		SQUIZER	01
		HARD BROOM	
7	HGL	SLESHA	01
		SQUIZER	01
		BRUSH NDOGO YA KUSUGULIA CHOO	01
8	PCB	SQUIZER	01
		JEMBE	01
		SOFT BROOM	01
9	HKL	JEMBE LENYE MPINI	01
		SLESHA	01
		SOFT BROOM	01

MAAGIZO MUHIMU YA VITABU VYA KIADA NA ZIADA

Ili mwanafunzi aweze kupata elimu bora na yenye kumwezesha kukabiliana na mazingira halisi; anapaswa kuwa na vitabu. Hapa ni baadhi ya vitabu ambavyo anapaswa kuja navyo ili aweze kumudu sawa sawa mchepuo wake.

1. **KISWAHILI**
   - *Kiswahili sekondari – Taasisi ya Elimu*
   - *Sarufi ns Fasihi – Sekondari na Vyuo (Felician Nkwera)*
   - *Nadharia ya Lugha- Chaja Masebo na N. Nyangwine*
   - *Tafsiri na Ukalimani – Wanjara*
   - *Nadharia ya Fasihi – J.A. Masembo*
2. **HISTORY**
   - *Mastering Advanced level History book I and II- Kato (2010)*
   - *Basic themes in European: Advanced level history paper I and II (Ismail Ngobi- 2012)*
   - *Major Events in African History paper I (FR. Jovitus F. Kamara)*
3. **ENGLISH LANGUAGE**
   - *Advanced literature*
   - *Advanced level literature an essential guide- Nicholaus Asheri*
   - *A man of the people by Chinua Achebe*
4. **COMMERCE**
   - *Text Book of Commerce – By Dinah*
   - *Essentials of Commerce for East Africa*
   - *Advanced level commerce*
   - *Commerce simplified*
5. **GEOGRAPHY**
   - *General geography in Diagrams (R.B. Bunnett)*
   - *Practical Geography for Africa (John M. Pritchard)*
   - *Physical geography for Africa (D.T. Msabila)*
   - *Human and Economic Geography (D.T. Msabila)*
6. **PHYSICS**
   - *Principles of Physics- Rogers Mancaster*
   - *Principles of Physics – Nelkon and Parker*
   - *Principles of Physics – Tom duncan*
7. **BIOLOGY**
   - *Advanced Biology for Secondary Schools – (Michael R.)*
   - *Biological Science – (Taylor O.J and Stoud G. W)*
   - *Cell structure and organization – L. Msaki*
   - *Understanding Biology- Fourth Edition*
8. **ADVANCE MATHEMATICS**
   - *Advanced level Mathematics – C.J. TRANTER*
   - *Pure mathematics 1 and 2*
   - *Mathematics for A- level (Volume 1 and 2) By S. Chands*
   - *Advanced level Mathematics (Vol 1) – L.K. Shayo*
9. **CHEMISTRY**
   - *Advanced level physical chemistry with general chemistry: APE network 2012, 1st Edition 2011*
   - *Essentials of physical chemistry- Arun Bahl*
   - *Organic chemistry: Arun Bahl, First Edition Illustrative Revised 2012*
10. **ECONOMICS**
    - *Economics paper one – By Ambilikile*
    - *Economics paper two – By Ambilikile*
11. **ACCOUNTS**
    - *Bussiness Accounting Volume – By Frank Wook*
    - *Bussiness Accounting Volume – By Frank Wook*
12. **GENERAL STUDIES**
    - *General Studies for Advanced level Certificate, Form six - Richard R.F. Mbalase*
    - *General Studies for Advanced level Certificate, Form five - Richard R.F. Mbalase*
    - *General Studies, Supplementary book for Advanced and Colleges, second edition- Konrad Adenaker Stiftung*

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MUSOMA.